


# MACHANJO INALINDAKA MAISHA

## Machanjo inatunzaka afya na kulinda maisha.

Mu inchi ya Amerika iko wakati mutu analazimishwa kuonyesha kama alipigwa chanjo. Kwa mfano kama batoto banakwenda ku masomo. Ao kama mutu anaomba kazi Fulani, ao kama anaomba kuishi ao kutembelea Amerika.




Machanjo iko mu dunia tangu miaka mamia. Machanjo inatukinga ku magonjwa mingi ya hatari kama vile sulua, polio, homa ya grippe, corona na ingine.

## Machanjo ilikinga batu mingi kuzidi matokeo ingine yote ya buganga.


Machanjo inafanyaka kazi mu mwili namuna kani? Machanjo iko salama na inazuiya bugonjwa. Inatayarisha mwili yako kutambua bilulu kama vile bakteria ao virusi.

Chanjo inafundisha mwili namuna ya kupigana na ambukizo mbele ya bilulu kukupatia bugonjwa. Kama vile mutoto anajifunza kusoma na kuandika, mwili pia unasoma na kukumbuka maelezo ya bugonjwa na kila chanjo.





**Kila chanjo iko na wakati yake, na kipimo yake, na siku yake ya kurudia tena kuchanjwa. Kwa mfano, kuna machanjo ya mutoto muchanga. Inginge ya mutu muzima, ingine ya muzee, ingine ya mwanamuke mwenye mimba.**



**Kuna machanjo ya kupigwa mara moja tu. Kuna machanjo ingine ya kupigwa kila mwaka kama vile chanjo ya homa ya grippe.**

**Kuna chanjo ya wakati mutu anakwenda safari fasi fulani.**

**Uko na maswali juu ya chanjo? Zungumuza na muganga wako. Anaweza kukuongoza vizuri juu ya machanjo gani wewe na familia yako munalazimishwa kupigwa.**



**Kumbuka hivi: machanjo ni dawa iko salama, ya mafa, na ya kutunza maisha. Familia mingi inaona chanjo kama alama ya kitumaini ya miaka ya mbele. Machanjo ni njia moja bora ya sisi kuweza kujilinda na kulinda familia yetu. Zungumuza na mganga wako leo!**